**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MSHARIKI**

**Dodoma**
30 Januari 2026

*Mawasiliano: gcu@nje.go.tz*

# TAARIFA KWA UMMA

## TAHADHARI KWA WATANZANIA DHIDI YA UTAPELI WA MTANDAONI KUHUSU FURSA ZA KAZI, BIASHARA NA MAFUNZO NJE YA NCHI

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inapenda kuutarifu umma wa Watanzania kuhusu kuongezeka kwa vitendo vya utapeli vinavyohusisha ahadi za fursa za kazi, biashara au masomo nje ya nchi, hususan kupitia watu binafsi au kampuni zisizo rasmi zinazodai kuwa na uhusiano na Balozi za Tanzania au wa nchi nyingine.

Wizara imebaini kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa baadhi ya Watanzania waliodaiwa fedha kwa ajili ya kugharamia maombi ya ajira, vibali vya kazi, visa, tiketi za ndege, bima au vibali vingine, ambapo baada ya kufanya malipo hayo, wahusika husitisha mawasiliano au hupotea kabisa. Aidha, baadhi ya matapeli hutumia barua pepe, mitandao ya kijamii au ujumbe wa *WhatsApp* wakijitambulisha kuwa mawakala halali au wawakilishi wa ubalozi.

Kutokana na hali hiyo, Wizara inapenda kutoa tahadhari na maelekezo yafuatayo kwa umma:

1. Hakuna Ubalozi wa Tanzania unaodai au kupokea fedha kwa ajili ya mtu kupata ajira, visa au fursa za mafunzo nje ya nchi kupitia watu au akaunti binafsi;

2. Wananchi wanashauriwa kutochukua hatua za kulipa fedha kwa ahadi za ajira nje ya nchi bila kufanya uhakiki wa kina;

3. Wananchi wanashauriwa kuepuka kufanya malipo kwa ahadi za ajira hususan ajira ambazo zimepatikana bila kufanya usaili wowote;

4. Kabla ya kuendelea na maombi yoyote ya kazi au ajira mtandaoni, wananchi wahakikishe taarifa hizo kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na

Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Ofisi *ya* Waziri Mkuu *Kazi*, Ajira na Mahusiano, au Ubalozi wa Tanzania uliopo katika nchi husika;

5. Wananchi wanatakiwa kuwa waangalifu na ujumbe unaotumwa kupitia baruapepe, *WhatsApp* au mitandao ya kijamii, hususan pale unapoombwa malipo ya haraka au taarifa binafsi zikiwemo za kibenki; na

6. Kwa taarifa au uthibitisho zaidi, wananchi wanahimizwa kuwasiliana na Ubalozi wa Tanzania au Ubalozi wa nchi husika uliopo Tanzania kwa njia rasmi.

**Imetolewa na:**
Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali